

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5

Fax No. +255 026 2322624

E-mail: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MWALIKO WA WADAU KUTOA MAONI
KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA HUDUMA ZA HABARI
(PUBLIC HEARING NOTICE)**

Katika kukamilisha majukumu yake ya kushughulikia **Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa mara nyingine tena imepanga kufanya mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau (*Public Hearing*) kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (9) kuhusu Muswada huo siku ya Jumamosi tarehe 29 Oktoba, 2016.

Mkutano huo wa Wadau (*Public Hearing*) utafanyika Mjini Dodoma katika Ukumbi uliopo Jengo la Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Ghorofa ya Tatu kuanzia Saa tatu Asubuhi. Wadau wote wa Maswala ya Habari wanashauriwa kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao kabla Muswada huo haujaingia katika hatua nyingine ya Utungaji Sheria. Aidha, maoni ya wadau yanaweza pia kuwasilishwa kwa njia ya posta au barua pepe kwa anuani ifuatayo pia:-

Katibu wa Bunge,

Ofisi ya Bunge,

S. L. P. 941,

DODOMA.

Barua pepe: cna@bunge.go.tz

Muswada huo unapatikana kwa kupakua (**downloadable**) katika tovuti ya Bunge la Tanzania ambayo ni www.parliament.go.tz .

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano

Ofisi ya Bunge

DODOMA

27 Oktoba, 2016